



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
WIZARA YA AFYA  
BARAZA LA FAMASI



## **TAARIFA KWA UMMA**

### **MABADILIKO YA TAREHE YA MITIHANI YA TAALUMA KWA WAHITIMU WA KOZI ZA FAMASI**

Ofisi ya Msajili ilitoa tangazo la mitihani ya taaluma kuwa itafanyika tarehe **22 - 24 Julai, 2026** kwa wahitimu wa kada za famasi wanaohitaji kusajiliwa na Baraza kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Famasi Sura 311.

Ofisi inapenda kuwataarifu wahitimu waliowasilisha maombi kuwa, mitihani hiyo imesogezwa mbele na itafanyika tarehe **29 - 31 Julai, 2026**. Pia, ofisi inapenda kuwafahamisha kuwa inaendelea kupitia na kuidhinisha maombi ya mitihani yaliyowasilishwa ili kuwezesha wahitimu kulipia na kupata namba ya mitihani.

Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe [info@pc.go.tz](mailto:info@pc.go.tz)/ [registration@pc.go.tz](mailto:registration@pc.go.tz) au Simu: 0736222503/0736222515.

**Imetolewa na;  
MSAJILI  
BARAZA LA FAMASI**